# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

Simu: +255262963470
Barua Pepe: ps@mit.go.tz
Barua Pepe: gcu@mit.go.tz
Tovuti: www.viwanda.go.tz

Mji wa Serikali, Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S.L.P 2996,
**40478, Dodoma**.

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## KATAZO LA KUWEKA ZAWADI, FEDHA TASLIMU, VOCHA AU KUPONI KWENYE MIFUKO YA BIDHAA ZA "WALL PUTTY"

**07/02/2025, DODOMA.**

Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara inatoa katazo kwa Wazalishaji, Wasambazaji wa bidhaa za "Wall Putty" kuacha kuweka zawadi, fedha taslimu, vocha, kuponi na vitu vingine tofauti na bidhaa ya *wall putty* ndani ya Mifuko kinyume na matakwa ya Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo zinazoelekeza kuzingatia viwango vya ubora wa bidhaa na ushindani wa haki na kutoathiri taswira ya Tanzania ambayo imefanikiwa kupata masoko ya bidhaa mbalimbali katika masoko ya ndani na nje ya nchi hususani kupitia Mikataba ya biashara baina ya nchi, kikanda na kimataifa kama vile EAC, SADC, AfCFTA, COMESA, AGOA.

Vitendo hivi ni kinyume na sheria zifuatazo:

i) **Sheria ya Viwango Sura ya 130** ambayo inatoa mamlaka kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kusimamia na kuhakikisha ubora wa bidhaa. Kuweka vitu visivyo sehemu ya bidhaa inaweza kuchukuliwa kama ukiukaji wa viwango vilivyowekwa.

ii) **Sheria ya Vipimo Sura ya 340** inayosimamia usahihi wa vipimo na uzito wa bidhaa. Kuongeza vitu kama zawadi au fedha kwenye bidhaa kunaweza kuathiri uzito halisi wa bidhaa na hivyo kukiuka sheria hii.

iii) **Sheria ya Ushindani Sura ya 285** inayokataza vitendo vyovyote vinavyoweza kupotosha watumiaji au kuathiri ushindani wa haki sokoni. Kuweka zawadi au vocha kwenye bidhaa kunaweza kuchukuliwa kama mbinu ya upotoshaji au ushindani usio wa haki.

Aidha, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Vipimo (WMA) zinatakiwa kuhakikisha bidhaa zote za *Wall Putty* zinazozalishwa zinakidhi ubora na viwango vinavyokubalika kabla ya kuingizwa Sokoni.

Msako mkali wa ukaguzi utaanza kufanyika na hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wazalishaji wanaoendelea kuweka vitu hivyo kuanzia **Machi 1, 2025**.

**Imetolewa na:**

Digitally Signed By Suzan Clement Mshakangoto
Fri Feb 07 16:59:02 EAT 2025

Suzan C. Mshakangoto
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Viwanda na Biashara